ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 32*** ***27th AUGUST, 2024***

***SPECIAL SUPPLEMENT***

*To The Special Gazette of the United Republic of Tanzania No.31 Vol. 105 Dated 27th August, 2024*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 752A la tarehe 27/8/2024

SHERIA YA SHUGHULI ZA RAIS,
(SURA YA 9)

# TANGAZO

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 4)*

SHUGHULI ZA RAIS (KUANZISHA NA KUTUNUKU NISHANI) MAREKEBISHO YA TANGAZO LA MWAKA 2024

Jina

TS. Na. 32 ya 2014

1. Tangazo hili litajulikana kama Shughuli za Rais (Kuanzisha na Kutunuku Nishani) Marekebisho ya Tangazo la mwaka 2024 na litasomwa pamoja na Shughuli za Rais (Kuanzisha na Kutunuku Nishani) Tangazo la mwaka 2014 ambalo hapa limerejewa kama "Tangazo kuu".

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

2. Tangazo kuu linarekebishwa katika Jedwali la Kwanza kwa kuongeza aya mpya baada ya aya ya 19 kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| "20. NISHANI YA MIAKA 60 YA JESHI LA ULINZI LA WANANCHI WA TANZANIA | Nishani hii itatolewa kwa wanajeshi wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania walioko kwenye utumishi tarehe 1 Septemba, 2024. | Nishani itakuwa ya dhahabu ya kuchovywa ya umbo la mfano wa nyota yenye kipenyo cha ukubwa wa *45mm*.<br><br>Katikati yake kutakuwa na mduara, ndani ya mduara kutakuwa na nembo ya Jeshi la |

Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na upande wake wa kushoto kutakuwa na mwaka 1964 na upande wake wa kulia kutakuwa na mwaka 2024.

Nishani itaning'inizwa kwenye kipande kilichonyooka cha chuma na utepe wenye upana wa *38mm* rangi za bendera ya Jeshi la Ulinzi ukiwa na tarakimu '60' katikati yake iliyoandikwa kwa dhahabu iliyochovywa.

Utepe wa Nishani hiyo utavaliwa kifuani upande wa kushoto wa shati.

Nishani itahifadhiwa katika kasha la ngozi ya rangi nyekundu iliyoandikwa kwa maandishi ya fedha.

Alama zake zimechapwa kwa ubora wa fedha.".

Limetolewa kwa saini yangu na kugongwa lakiri ya Umma leo tarehe 26 mwezi Agosti, 2024.

Ikulu,
Dodoma

SAMIA SULUHU HASSAN
*Rais*